

Sauti za Kiswahili - Sarufi na Matumizi ya Lugha Kiswahili Notes

- [Utangulizi](#)
- [Irabu \(Vokali\)](#)
 - [Matamshi/Uainishaji wa Irabu](#)
- [Konsonanti](#)
 - [Aina za Ala za Sauti](#)
 - [Matamshi/Uainishaji wa Konsonanti](#)

[Utangulizi](#)


- Kuna makundi mawili ya sauti za kiswahili:
 - Irabu (Vokali);
 - Konsonanti;

[Irabu \(Vokali\)](#)

a, e, i, o, u

- Sauti ambazo hutamkwa kwa ulaini bila hewa kuzuiliwa katika ala za sauti.

[Matamshi/Uainishaji wa Irabu](#)



- **a** ni ya katikati na chini kinywani na midomo ikiwa imeviringa.
- **e** ni ya mbele na kati kinywani na midomo ikiwa imetandazwa.
- **i** ni ya mbele na juu kinywani na midomo ikiwa imetandazwa.
- **o** ni ya nyuma na kati kinywani na midomo ikiwa imeviringa.
- **u** ni ya nyuma na juu kinywani na midomo ikiwa imeviringa.

[Konsonanti](#)

b, ch, d, f, g, h, j, k, l, m, n, p, r, s, t, v, w, y, z

- Sauti ambazo wakati wa kutamkwa hewa huzuiliwa katika ala za sauti.
- Kuna aina mbili kuu za sauti za konsonanti:

1. **Sauti Ghuna** - konsonanti hizi zinapotamkwa, hewa hutikisa nyuzi za sauti
2. **Sauti Sighuna** - konsonanti hizi zinapotamkwa, hewa haitikisi nyuzi za sauti

Aina za Ala za Sauti

Ala Tuli

- Ambazo hazisogei mtu akitamka k.m. meno, ufizi, kaa kaa gumu, kaa kaa laini na koo/koromeo.

Ala sogezi

- Ambazo husogea mtu akitamka k.m. midomo na ulimi.

Matamshi/Uainishaji wa Konsonanti

- Huainishwa kulingana na inapotamkiwa, kuwepo au kutokuwepo kwa mtetemeko katika nyuzi za sauti na jinsi hewa inavyozuiliwa katika ala k.m. /p/ ni ya midomo, kipasuo na sikhuna

	Midomo	Midomo+Meno	Meno+Ulimi	Ufizi	Kaaka+ufizi	Kaaka gumu	Kaaka laini	Koo	Aina ya sauti
Vipasuo	p			t		j	k		sighuna
	d			d			g		ghuna
Vikwamizo/Vikwaruzo		f	th	s		sh	gh	h	Sighuna
		v	dh	z					ghuna
Kipasuo - Kwamizo					ch				sighuna
Nazali/Ving'ong'o	m			n		ny	ng'		ghuna
Kitambaza				l					ghuna
Kimaden de				r					ghuna
Viyeyusho/Nusurabu						y	w		ghuna

Vipasuo

- Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa, huzuiliwa kabisa na kuachiliwa kwa ghafla na mpasuko mdogo kutokea.

Vikwamizo/Vikwaruzo

- Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa hupitishwa katikati ya ala kwa kukwamizwa.

Kipasuo kwamizo/kwaruzo

- Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa nje kwa nguvu, huzuiliwa kabisa halafu mwanya mdogo huachwa hewa ipite kwa kukwamizwa.

Nazali/Ving'ong'o

- Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa kuna kiasi cha hewa huachiliwa na kupitia puani

Kitambaza

- Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa kwa nguvu, kuzuiliwa na kuachiliwa